JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

# SERA YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

Imeandaliwa na:
**Halmashauri ya Manispaa**
S.L.P 1070
**LINDI**
Simu:+255023-220
Nukushi: +255 023-220-2116
Barua pepe: info@lindimc.go.tz
Tovuti: www.lindimc.go.tz

*Juni, 2024*

# YALIYOMO


YALIYOMO ..... i

DIBAJI ..... iii

MUHTASARI WA SERA ..... iv

VIFUPISHO VYA MANENO MUHIMU (GLOSSARY) ..... v

1.0: UTANGULIZI ..... 1

1.1: Dira ya Sera ..... 1

1. 2: Dhima ya Sera ..... 1

2.0: MALENGO MAHUSUSI YA SERA ..... 1

3.0: MISINGI YA UTEKELEZAJI ..... 1

4. 0: UUNDWAJI WA KAMATI MUHIMU ..... 2

5.0: MIKAKATI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA. ..... 3

5.1 (A) Jedwali linaloanisha Mikakati ya Kupambana na Rushwa ..... 3

(B) Maelezo ya Ziada: ..... 4

6.0: UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA SERA ..... 4

6.1: Wajibu wa Utekelezaji ..... 4

6.2: Ratiba ya Utekelezaji ..... 5

6.3: Ufuatiliaji na Tathmini ..... 5

6.4: Mawasiliano na Ushirikiano ..... 5

7.0: MAFUNZO NA UELEWA ..... 5

7.1: Malengo ya Mafunzo ..... 5

7.2: Walengwa wa Mafunzo ..... 5

7.3: Aina ya Mafunzo na Utoaji Wake ..... 6

7.4: Ushirikiano katika Mafunzo ..... 6

8.0: RASILIMALI ZA UTEKELEZAJI ..... 6

8.1: Bajeti ..... 6

8.2: Rasilimali Watu ..... 6

8.3: Rasilimali za Kifundi na Miundombinu ..... 6

9.0: UTEKELEZAJI WA SHERIA NA ADHABU ..... 6

9.1: Msingi wa Kisheria ..... 6

9 .2: Hatua kwa Watumishi ..... 6

10.0: TATHMINI YA HATARI ZA RUSHWA (RISK ASSESSMENT) ........ 7
10.1: Maana ya Tathmini ya Hatari ........ 7
10.2: Malengo ya Tathmini ya Hatari ........ 7
10.3: Mbinu za Kutathmini Hatari za Rushwa ........ 7
10.4: Eneo la Hatari za Rushwa Kwenye Manispaa ........ 7
10.5: Mikakati ya Kupunguza Hatari za Rushwa ........ 7
12.0: NYARAKA ZINAZOHUSIANA NA SERA ........ 9
12.1: Sheria na Kanuni Muhimu ........ 9
12.2: Miongozo na Mikakati ya Kitaifa ........ 9
12.3: Mikataba na Makubaliano ........ 9
12.4: Miongozo ya Ndani ya Manispaa ........ 9
TAMKO LA KURIDHIA ........ 10



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

## DIBAJI

Katika muktadha wa kujenga utawala bora na kuhakikisha utoaji wa huduma kwa uwazi, ufanisi na uadilifu kwa wananchi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kusisitiza umuhimu wa kudhibiti vitendo vya rushwa katika sekta zote za umma. **Kupitia Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa Awamu ya Nne (NACSAP IV 2023–2030)**, serikali inalenga kuimarisha mifumo ya uwajibikaji, uwazi na maadili katika taasisi zake, ikiwemo mamlaka za serikali za mitaa.

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, kama sehemu ya serikali za mitaa, inatekeleza wajibu wake kwa kuhakikisha inasimamia vyema rasilimali, inatoa huduma kwa viwango vya juu, na kuondoa mianya yote ya rushwa inayoweza kudhoofisha maendeleo ya wananchi. Sera hii ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeandaliwa ili kutoa mwongozo wa wazi na wa utekelezaji wa afua mbalimbali dhidi ya vitendo vya rushwa ndani ya Manispaa.

Sera hii inajumuisha dira, dhima, malengo mahususi, misingi ya utekelezaji, majukumu ya kamati za uadilifu na menejimenti, pamoja na mikakati ya kudhibiti maeneo hatarishi ya rushwa. Aidha, imesisitiza matumizi ya TEHAMA, ushirikiano wa wadau, mafunzo ya maadili, na ushiriki wa wananchi katika kufichua na kuzuia vitendo vya rushwa.

Natoa wito kwa watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, viongozi wa jamii, mashirika ya kiraia, taasisi binafsi, na wananchi kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa sera hii. Ushirikiano nadhamira ya dhati vitaiwezesha Manispaa ya Lindi kuwa taasisi inayozingatia maadili, haki na uwajibikaji wa kweli.



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

## MUHTASARI WA SERA

Sera ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ni nyenzo rasmi ya kuhakikisha kuwepo kwa mazingira yenye maadili, uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Sera hii imeandaliwa kwa kuzingatia **Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa Awamu ya Nne (NACSAP IV 2023–2030)** kwa lengo la kuweka mfumo endelevu wa kuzuia, kugundua na kuchukua hatua dhidi ya vitendo vyote vya rushwa na ukiukwaji wa maadili.

Dira ya sera ni kuifanya Manispaa ya Lindi kuwa taasisi ya umma isiyo na rushwa, inayotoa huduma kwa haki, ufanisi na kwa kuzingatia maadili ya uongozi bora. Dhima yake ni kuhakikisha kuwa kuna mfumo madhubuti wa kuzuia mianya ya rushwa kupitia mifumo ya utawala bora.

Sera hii inajumuisha malengo mahususi sita, misingi ya utekelezaji mitano, uundaji wa Kamati ya Uadilifu na Kamati Maalum ya Menejimenti, pamoja na mikakati ya wazi ya kudhibiti maeneo hatarishi ya rushwa kama vile manunuzi ya umma, ukusanyaji wa mapato, utoaji wa huduma, usimamizi wa rasilimali watu na ushiriki wa jamii.

Pia, sera inaweka utaratibu wa ufuatiliaji, tathmini, utoaji wa ripoti za utekelezaji, na elimu ya maadili kwa watumishi, viongozi na wananchi. Rasilimali za utekelezaji, sheria zinazotumika, pamoja na hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya wahusika wa vitendo vya rushwa zimefafanuliwa.

Kwa ujumla, sera hii inalenga kuimarisha uwajibikaji, kuongeza ufanisi wa huduma, kupunguza mianya ya rushwa na kujenga imani ya wananchi kwa taasisi za serikali kupitia mifumo madhubuti ya maadili na usimamizi bora wa rasilimali.



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

## VIFUPISHO VYA MANENO MUHIMU (GLOSSARY)

| Kifupisho | Maana Kamili kwa Kiswahili |
|---|---|
| CAG | Control and Audit General |
| NACSAP | National Anti-Corruption Strategy and Action Plan |
| NACSAP IV | National Anti-Corruption Strategy and Action Plan PHASE 4(2023–2030) |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| POS | Point of Sale mashine |
| PEPMIS | Performance Evaluation and Personnel Management Information System |
| NEST | National e-Procurement System of Tanzania |
| PMU | Procurement Management Unit |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| M&E | Monitoring and Evaluation |



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

## 1.0: UTANGULIZI

Rushwa ni adui mkubwa wa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Halmashauri kama ya Manispaa ya Lindi ni sawa na taasisi yoyote ambayo kama itamhusu uwepo wa mianya ya rushwa huathiri moja kwa moja utoaji wa huduma bora, usawa wa kiutawala, na kuondoa imani ya wananchi kwa mamlaka za serikali.

Katika kukabiliana na hali hii na kuhakikisha rushwa inakomeshwa, serikali ya Jamhuri ya Muungango wa Tanzania kupitia **Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne (NACSAP IV 2023–2030)** imedhamiria kuimarisha mifumo ya uwajibikaji, uwazi, na uadilifu katika ngazi zote. Manispaa ya Lindi, kama sehemu ya serikali za mitaa, inajukumu la kutekeleza sera na mikakati hii kwa vitendo.

### 1.1: Dira ya Sera

Manispaa ya Lindi kuwa taasisi ya umma isiyo na rushwa, yenye kutoa huduma kwa uwazi, kwa haki na kwa kuzingatia maadili ya uongozi bora.

### 1. 2: Dhima ya Sera

Kuweka mfumo madhubuti wa kuzuia, kugundua, na kuchukua hatua dhidi ya vitendo vyote vya rushwa na ukiukwaji wa maadili ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

## 2.0: MALENGO MAHUSUSI YA SERA

- Kuimarisha mifumo ya uwazi, uwajibikaji, na maadili katika utendaji kazi wa kila siku.
- Kuzuia mianya ya rushwa kupitia mifumo ya utawala bora.
- Kuunda kamati za uadilifu na menejimenti zitakazosimamia utekelezaji wa sera hii.
- Kuelimisha na kushirikisha watumishi wa umma na jamii kuhusu madhara ya rushwa.
- Kuimarisha ushirikiano kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na taasisi za kitaifa za kupambana na rushwa kama TAKUKURU, CAG n.k.
- Kuweka utaratibu mzuri wa kupokea, kuchunguza na kuchukua hatua juu ya malalamiko ya rushwa.

## 3.0: MISINGI YA UTEKELEZAJI

- Uwazi katika maamuzi na matumizi ya rasilimali
- Uwajibikaji wa kila mtumishi wa umma wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi
- Usawa wa kijinsia, haki na ushirikishwaji
- Ufuataji wa sheria, kanuni na taratibu
- Ushirikiano wa wadau (serikali, sekta binafsi, mashirika ya kiraia, wananchi)



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

## 4. 0: UUNDWAJI WA KAMATI MUHIMU

### 4.1. Kamati ya Uadilifu ya Manispaa

Kamati hii ni chombo muhimu chini ya NACSAP kinachowajibika katika kusimamia utekelezaji wa maadili, uwazi, na uwajibikaji.

#### 4.1.1: Majukumu ya Kamati ya Uadilifu

- Kusimamia utekelezaji wa sera hii.
- Kuanisha maeneo yenye vishawishi vya rushwa na kuandaa afua,
- kuanisha na kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa shughuli za taasisi zinazoshabihiana na Mkakati na kuzitolea taarifa kwenye Kamati Maalum ya Menenjimenti,
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za robo mwaka na mwaka kwa kamati Maalum ya Menejimenti,
- Kupokea, kuchambua na kushughulikia malalamiko kutoka ndani na nje ya Taasisi yanayotokana na ukiukwaji wa maadili. Kamati itachukua hatua ndani ya siku saba,
- Kuandaa na kutekeleza afua za kujenga uwezo kwa watumishi wa Taasisi juu ya maadili, kuthibiti rushwa na utawala bora,
- Kufuatilia utekelezaji wa mafunzo ya awali kwa watumishi wapya na watumishi waliopanda cheo/kuteuliwa,
- Kushauri menejimenti kuhusu masuala ya maadili, rushwa na utawala bora,
- Kuandaa na kutekeleza mpango kazi wa awamu ya Nne ya Mkakati.

#### 4.1.2: Muundo wa Kamati ya Uadilifu

- Mwenyekiti: Afisa atakaeteuliwa na Mkurugenzi
- Katibu: Afisa Mwandamizi kutoka idara ya Utawala na Rasilimali watu, na
- Wajumbe wengine watatu kati ya hao mmoja anatakiwa kutoka nje ya Halmashauri.

### 4.2: Kamati Maalum ya Menejimenti

Kamati hii itapokea,kujadili na kushauri mamlaka kwa masuala yahusuyo utekelezaji wa mkakati.Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa msimamizi mkuu wa utekelezaji wa awamu ya Nne ya Mkakati akishauriwa na Kamati Maalum ya taasisi ambayo inaundwa na Wakuu wa Idara na Vitengo.

#### 4.2.1: Muundo wa Kamati Maalum ya Menejimenti

- Mwenyekiti: Mkurugenzi wa Manispaa
- Katibu: Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu
- Wajumbe: Wakuu wa Idara na Vitengo
- Mwenyekiti wa Kamati ya uadilifu;atakuwa mjumbe mwalikwa.



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

4.2.2: Majukumu ya Kamati Maalum ya Menejiementi

- Kuhakikisha Kamati ya Uadilifu inaanzishwa na kufanya kazi kwa kuzingatia mfumo wa ufuatiliaji tathmini na kujifunza
- Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Mkakati unajumuishwa kwenye mpango kazi na bajeti ya mwaka ya Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza malengo mahususi ya Mkakati pamoja na afua zianzolengwa.,
- Kuandaa, kuthibitisha na kutekeleza Sera ya Taasisi dhidi ya Rushwa,
- Kuhakikisha watumishi wanazingatia sheria, kanuni, taratibu, pamoja na miongozo inayosimamia maadili ya utaalamu
- Kuchukua hatua muhimu za kudhibiti aina zote za rushwa, makosa ya kiutawala, na vitendo vya ukiukwaji wa maadili,
- Kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu ya Taasisi
- Kuanzisha mfumo wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi wenye kuzingatia usiri. Mfumo huo utakuwa na uwezo wa kupokea na kutoa mrejesho kwa mhusika ana kwa ana au kwa njia ya kitecknolojia ya kidigitali.
- Kujumuisha matokeo ya tathmini ya athari za rushwa kwenye daftari la usajili wa vihatarishi na,
- Kupokea na kupitia taarifa za robo mwaka kutoka kwenye Kamati ya uadilifu na kuziwasilisha kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

## 5.0: MIKAKATI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA.

5.1 (A) Jedwali linaloanisha Mikakati ya Kupambana na Rushwa

| Na. | Eneo lenye Hatari ya Rushwa | Mikakati ya kuzuia na kupambana na Rushwa | Wadau Wanaohusika |
|---|---|---|---|
| i. | Mnunuzi | Kuimarisha matumizi ya mfumo wa Kielectronic wa manunuzi wa wazi ( NEST) | Kitengo cha ununuzi |
| | | Kuonyesha matokeo ya zabuni kwa uwazi(Public notice board/tovuti) | Mkaguzi wa ndani |
| | | Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa michakato ya ununuzi na mikataba | Kamati ya Zabuni |
| ii. | Ukusanyaji wa mapato ya ndani | Kuepuka miamala ya pesa taslimu kwa kutumia TEHAMA (POS, mfumo wa malipo wa mtandao) | Idara zote zianatoa huduma |
| | | kufanya ufuatiliaji na upimaji wa mara kwa mara wa taarifa za fedha | Kitengo cha TEHAMA |
| | | Kuweka viwango vya ada wazi kwa wananchi | Kitengo cha Fedha |

| | | | |
|---|---|---|---|
| iii. | Maadili ya Watumishi | Kufanya mafunzo ya mara kwa mara kuhusu maadili na wajibu wa watumishi wa umma | Idara ya Utawala na Rasilimali watu |
| | | kutumia PEPMIS kupima utendaji na tabia kazini | Kamati ya Uadilifu |
| | | Kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa Maadili ya Utumishi wa Umma | Vyama vya wafanya kazi |
| | | kupunguza mwingiliano wa moja kwa moja kati ya watumishi na wananchi kwa kutumia huduma za mtandao | |
| iv. | Utoaji wa huduma kwa wananchi | Kuweka sanduku la maoni, na mfumo wa kidigitali wa maoni | Idara zote zianatoa huduma |
| | | Kutoa taarifa kwa umma juu ya haki zao na taratibu za kupata huduma | Kitengo cha TEHAMA |
| | | kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu miradi ya maendeleo (gharama, muda, mkandarasi n.k) | Kitengo cha Mawasiliano Serikalini |
| v. | Ushiriki wa Jamii | Kushirikisha wananchi kwenye upangaji, utekelezji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo) | Maafisa Kata na Mitaa |
| | | kuwezesha vikao vya wazi vya kupokea maoni ya jamii | Idara ya Mipango |
| | | Kuwezesha vikao vya wazi vya kupokea maoni ya jamii | Viongozi wa jamii na Asasi za Kiraia |

(B) Maelezo ya Ziada:

- Mikakati hii inatakiwa kuingizwa katika mipango ya kazi za kila Idara na Vitengo husika
- Kamati ya Uadilifu itasimamia utekelezaji wa mikakati hii kwa kushirikiana na Kamati Maalum ya Menejimenti,
- Tathmini ya utekelezaji itafanyika kila baada ya miezi mitatu na matokeo kuripotiwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa na TAKUKURU

## 6.0: UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA SERA

6.1: Wajibu wa Utekelezaji

- **Mkurugenzi wa Manispaa ya Lindi** atahakikisha sera hii inatekelezwa kwa ufanisi kupitia usimamizi wa karibu.
- **Kamati ya Uadilifu** itasimamia utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya sera.
- **Kamati Maalum ya Menejimenti** itatoa ushauri na kusaidia katika kutatua changamoto za utekelezaji.



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

6.2: Ratiba ya Utekelezaji

- Mikakati ya sera hii itatekelezwa kwa awamu za mwaka na tathmini itafanyika kila robo mwaka.
- Ripoti za maendeleo na changamoto zitatolewa kwa Kamati Maalum ya Menejimenti na kisha kwa Mkurugenzi.
- Mkurugenzi atawasilisha taarifa za utekelezaji za kila robo na mwaka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

6.3: Ufuatiliaji na Tathmini

- Kamati ya Uadilifu itahakikisha ufuatiliaji wa utekelezaji na kutoa mapendekezo ya maboresho.
- Ripoti za ufuatiliaji zitawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa na Katibu Mkuu Kiongozi kama inavyotakiwa.
- Tathmini ya athari za sera itafanywa kila baada ya mwaka mmoja ili kuhakikisha malengo yanatimia.
- Mapendekezo ya maboresho kutoka kwa watumishi,wadau na wananchi yatatathmiwa na kuingizwa kwenye sera kila baada ya miaka mitatu (03)

6.4: Mawasiliano na Ushirikiano

- Manispaa itahakikisha ushirikiano na taasisi za kupambana na rushwa kama TAKUKURU, CAG na vyombo vya sheria.
- Pia itahamasisha ushiriki wa wananchi na wadau wa maendeleo katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji.

## 7.0: MAFUNZO NA UELEWA

7.1: Malengo ya Mafunzo

Lengo kuu ni kuwajengea uwezo wadau wote wa Manispaa ya Lindi ili waweze kutambua, kuzuia, na kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya rushwa kwa kuzingatia sheria, kanuni, na miongozo inayosimamia maadili ya utumishi wa umma.

7.2: Walengwa wa Mafunzo

Mafunzo yatawahusisha makundi yafuatayo:
- Watumishi wa Umma wote wa Manispaa
- Viongozi wa Jamii (ngazi ya Kata, Mitaa)
- Mashirika ya kiraia na asasi zisizo za kiserikali
- Wananchi na wadau wa maendeleo



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

7.3: Aina ya Mafunzo na Utoaji Wake

- Mafunzo ya awali kwa watumishi wapya.
- Mafunzo endelevu kwa watumishi waliopo na viongozi wa jamii.
- Semina, warsha, na mikutano ya hadhara kwa wananchi.
- Elimu kwa njia ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

7.4: Ushirikiano katika Mafunzo

Manispaa ya Lindi itashirikiana na taasisi za maadili na kupambana na rushwa kama:

- TAKUKURU
- Ofisi ya Rais - TAMISEMI
- Taasisi za elimu na mafunzo
- Asasi za kiraia (CSOs)

## 8.0: RASILIMALI ZA UTEKELEZAJI

8.1: Bajeti

- Manispaa ya Lindi itatenga bajeti maalum kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati ya Sera hii.

8.2: Rasilimali Watu

- Maafisa wa Maadili
- Maafisa TEHAMA
- Wakaguzi wa ndani
- Wakufunzi wa maadili na sheria

8.3: Rasilimali za Kifundi na Miundombinu

- Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kupokea taarifa, kutoa elimu na kusimamia uwazi.
- Vifaa vya ofisi na vifaa vya mawasiliano kwa ufanisi wa utekelezaji wa Sera.

## 9.0: UTEKELEZAJI WA SHERIA NA ADHABU

9.1: Msingi wa Kisheria

Rushwa ni kosa la jinai linaloelezwa chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329.

9 .2: Hatua kwa Watumishi

Watumishi wa Manispaa ya Lindi watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa:



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

- Watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma.
- Watafikishwa kwenye vyombo vya sheria kwa uchunguzi na mashitaka.

- Wanaotoa taarifa dhidi ya rushwa watapewa ulinzi wa kisheria kulingana na miongozo ya TAKUKURU

## 10.0: TATHMINI YA HATARI ZA RUSHWA (RISK ASSESSMENT)

10.1: Maana ya Tathmini ya Hatari

Tathmini ya hatari za rushwa ni mchakato wa kutambua, kuchambua na kutathmini maeneo au shughuli katika Manispaa ya Lindi ambapo kuna uwezekano mkubwa wa kutokea vitendo vya rushwa.

10.2: Malengo ya Tathmini ya Hatari

- Kubaini maeneo yenye mianya ya rushwa ndani ya Manispaa.
- Kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia na kupambana na rushwa katika maeneo yaliyo hatarini zaidi.
- Kuimarisha mifumo ya usimamizi na uwazi katika utendaji kazi wa kila idara.

10.3: Mbinu za Kutathmini Hatari za Rushwa

- Kuchunguza taratibu na michakato ya utendaji kazi.
- Kufanya mahojiano na watumishi na wananchi.
- Kutathmini taarifa na malalamiko yaliyopo.
- Kutumia matokeo ya ukaguzi wa ndani na wa nje.

10.4: Eneo la Hatari za Rushwa Kwenye Manispaa

- Manunuzi na zabuni za bidhaa na huduma.
- Ukusanyaji wa mapato ya ndani.
- Utoaji wa huduma kwa wananchi.
- Usimamizi wa rasilimali watu.
- Usimamizi wa miradi ya maendeleo na mipango.

10.5: Mikakati ya Kupunguza Hatari za Rushwa

- Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika manunuzi na ukusanyaji mapato.
- Kuanzisha na kuendeleza mifumo ya uwazi katika kila hatua ya utoaji huduma.
- Kuendesha mafunzo endelevu kwa watumishi kuhusu maadili na sheria za rushwa
- Kuimarisha ushirikiano na vyombo vya usalama na taasisi za kupambana na rushwa.



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

## 11.0: HITIMISHO

Sera hii ni nyenzo muhimu ya kuhakikisha kuwa Manispaa ya Lindi inakuwa taasisi ya umma inayozingatia maadili, inayoepuka rushwa, na kutoa huduma bora kwa ufanisi. Utekelezaji wa sera hii unahitaji ushirikiano wa kila mtumishi, kiongozi na mwananchi. Kwa pamoja, tutaweza kujenga jamii yenye uwazi, uadilifu na maendeleo ya kweli.
Sera hii inaanza kutumika kuanzia tarehe **01 Julai 2024** baada ya kuidhinishwa na Mamlaka husika.



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

## 12.0: NYARAKA ZINAZOHUSIANA NA SERA

12.1: Sheria na Kanuni Muhimu

1. **Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329** – Sheria kuu inayozuia vitendo vya rushwa nchini Tanzania.
2. **Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298** – Inatoa miongozo kuhusu maadili na nidhamu kwa watumishi wa umma.
3. **Sheria ya Mifumo ya Serikali za Mitaa, Sura 287** – Inasimamia utendaji na mamlaka ya Halmashauri za Manispaa.
4. **Sheria ya Uhifadhi na Ulinzi wa Habari za Serikali, Sura 345** – Inahakikisha uwazi na usiri katika utoaji wa taarifa.
5. **Sheria ya Huduma za Umma (Access to Information Act)** – Inahakikisha wananchi wana haki ya kupata taarifa za umma.
6. **Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022**-Inahakikisha Watumishi wanafanya kazi kwa kufuata misingi ya haki, uwajibikaji, uwazi na utii kwa Serkali na Wananchi.

12.2: Miongozo na Mikakati ya Kitaifa

1. **Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa (NACSAP) Awamu ya Nne** – Mkakati wa kitaifa unaoendana na sera hii.
2. **Mwongozo wa Maadili ya Utumishi wa Umma** – Unaelekeza miongozo ya tabia na maadili kwa watumishi wa umma.
3. **Mwongozo wa Usimamizi wa Malalamiko ya Umma** – Unaelekeza jinsi ya kusimamia malalamiko kwa njia ya uwazi na wepesi.
4. **Miongozo ya matumizi Kidigitali katika utoaji wa huduma na uendeshaji wa shughuli za Serikali**- Unaelekeza matumizi ya teknolojia katika utawala bora.

12.3: Mikataba na Makubaliano

1. **Makubaliano na Taasisi za Kupambana na Rushwa (TAKUKURU,GSO, CAG)** – Mikakati ya ushirikiano wa pamoja katika kukabiliana na rushwa.
2. **Mikataba ya Ushirikiano na Asasi za Kiraia na Vyombo vya Habari** – Kuwezesha ufuatiliaji na uwajibikaji katika utoaji wa huduma.

12.4: Miongozo ya Ndani ya Manispaa

1. **Kanuni za Uendeshaji wa Halmashauri**-Inatoa mwelekeo wa utoaji wa huduma bora wenye kufuata misingi ya uwajibikaji na uadilifu kwa kuzingatia matakwa ya kanuni za ndani ya halmashauri.
2. **Mpango Mkakati wa Halmashauri (Strategic Plani)**-Unahahakisha utekelezaji wa Sera inazingatia malengo ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.
3. **Mkataba wa huduma kwa mteja**-Inatumika kama nyenzo ya upimaji wa huduma zinazotolewa kwa Wananchi wa Manispaa ya Lindi



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

## TAMKO LA KURIDHIA

Mimi, **Juma A. Mnwele**, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, ninathibitisha kuwa sera hii ya "Kuzuia na Kupambana na Rushwa" imeandaliwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mamlaka ya serikali za mitaa. Sera hii inalenga kuimarisha uwajibikaji, uwazi na maadili katika utendaji kazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi bila vitendo vya rushwa.

Ni wajibu wa kila mmoja kwa nafasi yake, Mtumishi, Kiongozi, wananchi na washiriki wa jamii kuhakikisha anatekeleza Sera hii kikamilifu kwa maslahi mapana na maendeleo endelevu ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Sera hii inaanza kutekelezwa kuanzia **tarehe 01 Julai 2024** baada ya kuwa imeridhiwa na Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Juma A. Mnwele

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI,**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA
LINDI



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz